



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE



(Barua zote ziandikwe Kwa Mkurugenzi Mtendaji)

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. **HWC/M.15/1/VOL III/93**

Tarehe: 17/05/2024

BETHA ANDREW BUGUMBA,  
S.L.P 408,  
**DAR ES SALAAM.**

### YAH:UTARATIBU WA KUANZA UZALISHAJI

Mada hapo juu yahusika.

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze ilipokea barua kutoka kwa Katibu Mtendaji Tume ya Madini inayokutambulisha kuwa mmiliki wa Leseni Na **PML 2697DSM - PML 2702DSM** zilizobainisha uchimbaji wa madini ya Kokoto.
3. Baada ya kufanya ukaguzi katika eneo lako na kupitia nyaraka ulizonazo ikiwemo taarifa ya Utunzaji wa Mazingira, Mihtasari ya Kijiji na uthibitisho wa umiliki wa eneo, Ofisi ya Mkurugenzi inatambua uwepo wako katika kijiji cha **PongweMsungura**.
4. Unatakiwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na Halmashauri ya wilaya ya Chalinze na kuhakikisha unatunza na kuhifadhi Mazingira wakati wote utakapokuwa unatekeleza shughuli zako, ikiwa ni pamoja na kulipa ushuru wa Halmashauri kwa wakati. Aidha unatakiwa kuendelea na mchakato wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) kwa mujibu wa sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 na hatimae kupata cheti cha Mazingira kutoka Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.
5. Nakutakia utekelezaji mwema.

  
Ramadhani S. Possi  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**CHALINZE.**

